# BARUA KWA MOYO WANGU

## NA HADITHI NYINGINE

**Wahariri**
Kaka FRED
John Ustadh Kamau

# BARUA KWA MOYO WANGU

*Na Hadithi Nyingine*

**© ELONGO PUBLISHERS 2022**

Imechapishwa kwa mara ya kwanza 2022

Haki zote zimehifadhiwa. Ni marufuku na hatia kwa wenye silika za kugushi, kuiga, kubadili, kuchapisha, kutafsiri, kuigiza au kutumia mbinu zozote bila idhini ya waandishi kupitia kwa wakili wao.

Mtu yeyote atakayefanya kitendo chochote kinyume cha sheria ataweza kushtakiwa.

**ISBN 979-8390-47-844-8**

**Wahariri**

Kaka Fred: +254716349065

Baruapepe: kakafred25@gmail.com

John Ustadh Kamau: +254711879421

Baruapepe: ustadhkamauelimu110689jk@gmail.com

# YALIYOMO


YALIYOMO ....................................................................................................iii

**DIBAJI** ........................................................................................................iv

ASILI YA UCHAWI na *Ustadh Kamau*............................................................ 5

BARUA KWA MOYO WANGU na *Bi Esther Wachira***Error! Bookmark not defined.**

MWISHO WA MWANZO na *Jeremiah Atulo*...**Error! Bookmark not defined.**

MAKOVU YA PENDO na *Caroline Mabosio*...**Error! Bookmark not defined.**

UTUMWA WA UHURU na *Bi. Enata Mulamu***Error! Bookmark not defined.**

HATUPO ULIPOTUACHA na *Kaka Fred*.......**Error! Bookmark not defined.**

ZIMENIZIKA na *Mwalimu Nyakundi* ............**Error! Bookmark not defined.**

DHIKI YA FARAJA na *Linda Kagoitsi*.............**Error! Bookmark not defined.**

MAREJEO YA NGAMANI na *Khayota Amos* .**Error! Bookmark not defined.**

CHUDI NA TALANTA na *Ndombi C. Wawire***Error! Bookmark not defined.**

WAJA WALA UHURU na *Wanjohi P. Mugambi***Error! Bookmark not defined.**

KIPI KIZURI na *Moreen Muhonja*...................**Error! Bookmark not defined.**

MAKABURI YENYE DHAHABU na *Silas Kemboi***Error! Bookmark not defined.**

MZALENDO na *Matheri D.N*..........................**Error! Bookmark not defined.**

ARUDI KWAO na *Sam K. Kanyoi*.....................**Error! Bookmark not defined.**

SHEREHE.........................................................**Error! Bookmark not defined.**

# DIBAJI

Mchonga mwiko hukimbiza mkonowe. Hii ina maana kuwa mja hulishughulikia jambo ili aje afaidike baadaye. Moyo husetiri mambo mengi sana mengine ya kuatua, kuajabia, kufurahia n.k Kila aamkaye alfajiri huwa na nia ya kuwahi chambo cha kusetiri tumbo. Antholojia hii itakupa nyenzo muafaka za kauli hii. Barua kwa Moyo Wangu na Hadithi Nyingine imemiliki uhalisia wa jamii ya leo. Wahusika wamechorwa ili kunasa ujumbe unaodhamiriwa. Hadithi zote zimehaniki masuala yanayofanyika katika kizazi hiki cha wanaleo na mazingira yake.

Wandishi wametupa mbinu chanya ya kukabili sampuli ya visa hasi. Maudhui mengine kama: usaliti, elimu, ufisadi, taasubi, udhalimu, nidhamu na mengine yamekusanywa na kuwekwa kwenye chombo kimoja. Kazi kwako msomi.

Antholojia hii imepaliliwa na waandishi kutoka janibu tofauti tofauti hapa Kenya. Matumizi ya tamathali yametumika vyema ili kumkuza msomaji kwa maneno mapya yatakayoujenga ukwasi wa lugha na mazungumzo yake. Ama kweli mwana mtambaa kule humshinda mzee wa kale.

Isake antholojia hii uonje mapishi yenye virutubishi vyote vitakavyokuacha na afua njema katika umilisi wa lugha ya Kiswahili. Usiteme utamu.

***Kaka Fred na John Kamau***
*Wahariri.*

# **ASILI YA UCHAWI na *Ustadh Kamau***

John Kamau almaarufu Ustadh Kamau (MALENGA MFAWIDHI) ni ali wa gatuzi la Nyeri. Ni mwalimu wa miaka mingi wa Kiswahili katika shule za msingi, upili na vyuo vya walimu. Ustadh ni mwandishi mtajika na mchanganuzi wa Kiswahili redioni na runingani. Ni mtunzi stadi wa mashairi. Ameandika vitabu na kushiriki katika sanaa ainati mathalanii: *Kigezo cha Msamiati* na *diwani ya Dunia ya pili, Mwamba wa Dhahabu na Hadithi Nyingine na Zawadi ya Baba na Hadithi Nyingine.* Ni mhariri wa Kitovu cha Hadithi.

Je, nuru na giza ni kipi hutangulia kingine? Je, ni kipi hufukuza kingine? Mwangaza na giza ni kipi chenye nguvu zaidi? Kuna tofauti gani kati ya usiku na mchana? Ikiwa mabaya hutekelezwa usiku na mazuri hutekelezwa mchana, basi tunaweza kudai kuishi ni kwa mchana tu? Je, kati ya usiku na giza ni kipi cha kuogopwa basi? Ni nani aliyeumbua maumbile ya Mungu na kuufanya usiku kuwa joho la kuficha mabaya? Ikiwa kuna mambo huogopwa ni maradhi. Naam! Maradhi humnyima mtu amani na raha. Kisha kuna kifo. Kifo kingalikuwa adui aonekanaye, hata wakembe wasioweza kutembea wangekikimbia. Aidha utasikia wengine wakisema, "mimi naogopa uji moto sana." Wengine watasema filamu za kuogofya almaarufu '*horror'*. Hata hivyo, huo ni uzushi tu kulingana na Rosa. Yeye anaogopa kitu tofauti kabisa. Anaamini kwamba ndicho chanzo cha maovu yote. Kwa maoni yake, wengi hukaa kutwa wakisubiri kitu hiki ili waanze mabaya waliyowapangia wenzao. Anashangaa kwa nini binadamu baada ya kutarazaki na kusumbuka kutwa nzima asijipumzishe ili kutafaraji. Anashindwa kuelewa kwa nini mja asitulize mawazo ili kupata nguvu mpya ya keshoye. Eti wakati wa usiku ndio waja wanafaa kutembeleana, kutagusana, kujuliana hali na kuliliana haja ili kueneza upendo. Ajabu kwamba ndio wakati dhuluma, chuki, fitina, ukorofi, umbeya, kisasi na fuska mbalimbali huendelezwa kwa nguvu za ajabu. Ama kweli Ibilisi wa mtu ni mtu. Chawa aumaye yu ubindoni mwa ndani. Kiza ndicho mzizi wa uhasama eti. Lawama zote akizibeba shetani huku tukisema ni mapenzi ya Mungu. Pukachaka! Mtu atafanya mabaya kisha akipatikana amlaumu shetani.

***

Rosa alikimbia upeo wa kukimbia. Maskini vijiguu vyake vidogo vilipiga njia mipigo sawia na ile ya kijoyo chake kidogo. Kijishanta chake kilipigapiga mgongoni kuhesabu hatua alizopiga katika safari yake. Safari aliyoizoea ya kutoka shuleni kuelekea nyumbani. Akifanya kasi ili kuwahi ratiba ya mambo iliyomsubiri macho wazi nyumbani. Fauka ya kufua kijisare chake kilichochanikachanika na kupauka rangi, alifaa kuwafulia nduguze pia – ndugu waliochangia kuyatia maisha yake bughudha. Kisha akame mbuzi watatu, awatafutie nyasi au majani mengineo mradi yakidhi haja. Ilimpasa pia kupika, kuosha vyombo, kufagia na kusafisha hata pasiposafishika. Ratiba ilijaa matukio yaliyojipanga shelabela. Ulikuwa wajibu wake Rosa-kitoto cha miaka thenashara-kujua ni shughuli ipi ilifaa kutangulia nyingine. Aidha amri za mama yake wa kambo, ambazo tangu hapo zikitolewa ama kwa ishara, au kwa majibu magumu kuelewa, hazikuwa za kuonyeshwa meno. Mama mtu angeivunja glasi kwa kuitazama tu.

Si mara moja Rosa alipojipata katika hali ya kuchagua kati ya: kuliwa, kutafunwa au kumezwa alipochelewa au kuchelea kuanza shughuli hii au ile. Vipigo na matusi aliyopata indigo yaliyomfunza. Akajua na ikamjuzu kuwa haikujalisha aanze au amalizie kwa hamkani gani. Kibwagizo chake siku zote kikawa kuwa, likupigalo ndilo likufunzalo. Lililokuwa muhimu ni kumaliza shughuli zote kabla ya malkia wa nyumba kuwasili. Mkazahau wake alikuwa kiumbe wa maumbile adimu. Huruma na toba ya shufaa kwake ulikuwa msamiati uliochopekwa kimakosa kamusini. Aisee! Mama mtu angekipinda chuma kwa kukitazama tu. Huyu ndiye majaaliwa yaliyomjalia Rosa. Binadamu mgumu na adhimu kuishi naye. Eti amlee, amwongoe, amwokoe na amtoe kwenye lindi la ukiwa na upweke. Maskini heri jaala ingejua kuwa ilikuwa ikimtumbukiza katika kina cha wivu na maumivu yenye wingi wa fazaa na fadhaa.

*****

Wazazi wake Rosa walikuwa wametangulia mbele za haki miaka miwili iliyokuwa imepita. Miaka hiyo miwili kwake Rosa alikiona kiza asichowahi kukiona katika dunia yake. Akiwa angali mdogo wa kimo na umri. 6 amauti6e zilizotolewa siku za mazishi na maziko ya wazazi wake angali anazikumbuka hadi leo. Kila mpito wa dakika anabaki kuiona dunia ilivyo. Kila aliyezungumza siku hiyo alitoa ahadi za aiskrimu. Haijalishi cheo au umri. “Huyu mtoto mmoja hatatushinda. Tutamchukua

kwa ari na hiari." Alisema chifu siku ya mauko ya wazazi wake Rosa. Mwalimu mkuu wa shule aliyosomea Rosa hakusazwa, "Tutampa kisomo cha msingi na cha juu. Atasoma hadi kilele na kileleta cha elimu." Akidhani kuwa angaa kasisi Thomas angebaki msaada wa pekee, huyooo…, akahamishiwa eneo jingine na dhehebu alilotumikia la Kianglikani. Ama kweli hakuna msiba usiokuwa na mwenziwe.

Wakili wa wazazi wake bwana Kizito hakupewa nafasi aongee. Si maombolezini si mazikoni. Bwana Kizito alikuwa miongoni mwa watu wachache waliobaki duniani ambao mikono yao iliunguzwa na hongo. Koo lake lilikataa katakata kumeza hiki wengi wakiitacho chai. Hivyo basi, iliaminika kuwa, maharimu wa kuukeni na kuumeni walipojaribu kumpa chai alikatalia. Ikizingatiwa kuwa wazazi wake Rosa walikuwa wafanyakazi wa serikali, bima ya fidia 7 amauti yao ilikuwa donge nono. Kadiri wakili alivyoendelea kupambana kufa kupona ili fidia imfaidi mwanamkiwa, ndivyo matukio yalivyochacha. Miezi mitatu haikuisha, maskini wakili akaanza kujizungumzia mwenyewe. Baadaye akawa anavalia tai na bombo pekee. Watu wa aila yake walipoona maji yamezidi unga, wakamwondolea mbali kumnyimisha aibu. Msaidizi wake alipojaribu kuendeleza juhudi zake Kizito, akajipata taabani pia. Alianza kwa kufura koo. Akawa hamezi hatemi. Mwishowe akajifia. Hapo ndipo wanakijiji wa Kitovuni walipoanza kusema chini kwa chini. Aidha, hawakuwa wamesahau jinsi wazazi wa Rosa walivyoaga dunia kiajabuajabu tu.

***

"Ili kurahisisha mambo itabidi mhusika mkuu aondolewe. Kata pua uunge wajihi. Tena ni kitoto kidogo. Hakutazuka maswali mengi. Tuliweza kuchinja iwe vipi tushindwe kunyonga? Wewe ni mtaalamu wa mambo haya. Yapange yalainike." Rosa alisikia mjadala huu baina ya mkazahau wake Bi Kovu na Bi Khadija aliyekuwa shangazi yake Rosa jioni moja. Kwake Rosa hakujenga maudhui mazito kutokana na mjadala huo. Aliona kuwa haikumhusu kitu. Tena ikizingatiwa kuwa ulikuwa mkutano wa wahusika wawili kutoka pande zote mbili za familia. Aliona kuwa kulikuwa na mtu aliyekuwa amewakosea hao wawili na hivyo walitaka kulipiza kisasi. Hata Rosa alipoenda kulala siku hiyo, alimsikitikia sana yeyote huyo. Maskini asijue kuwa, Kikulacho ki nguoni mwako na ajuaye ulalapo ni nduguyo.

***

Siku hazikusimama. Rosa naye akaendelea kutia fora masomoni. Nduguze mabinamu wakamshangaa alivyokata masomo kwa mkato mmoja. Visu vyao butu, fitina na wivu vikawa vizingiti vikuu kwa Rosa kuwafaa. Angewasaidiaje mateja wahuni waliokuwa wamemezwa na michezo ya kamari na uraibu wa vijitembe walivyomeza? Rosa aliwashtakia kwa mama yao akachoka. Kuwaonya yeye kulikuwa sawa na mlevi kujaribu kutia uzi kwenye tundu la sindano. Aidha, angewanasihi vipi na walimwona Rosa kama kijakazi wao? Hali kwamba baba yao alikuwa akitarazaki mbali na nyumbani iliwafanya kuvimba vichwa wakawa hawaambiliki katu. Tena hata huyo baba akifika- aghalabu mara mbili kwa mwezi- hana usemi wowote mbele ya mkewe. Ama kweli, heri chungu huvunjika vigae, mtu huharibika asifae.

Siku ya siku ya kutibuka mambo ilimpata Rosa majilisini. Alikuwa ameitwa na mwalimu wake wa darasa. Ujumbe ulikuwa kwamba Bi Kovu alikuwa amepitia shuleni adhuhuri hiyo na kupata ruhusa ya Rosa kwenda nyumbani mapema. Si mara moja Rosa alijipata katika ruhusa ya kulazimishwa. Kazi zilipomzidi mlezi wake nyumbani, alitaka ruhusa ya Rosa akidai kuwa alitaka kumpeleka Rosa kwa mshaurinasaha ili apate utulivu kwa kufiwa. Nao walimu walifurahia sana utu wa Bi Kovu. Maskini wangalijua! Fauka ya kufanyizwa kazi za sulubu na shokoa, Bi Kovu alitaka Rosa akose baadhi ya masomo ili kupunguza makali yake masomoni. Hayo tisa, la kumi ni kuwa siku hii alikuwa na mengine. Rosa alifika nyumbani kama ilivyokuwa ada yake. Kinyume na siku nyingine, siku hiyo Bi Kovu alikuwa amepika na kupakulia chakula cha wali wa pukute kwa mboga kwenye sahani tatu. Moja ikawa jikoni na nyingine mbili kabatini.

Kwake Bi Kovu, alidhani kuwa Rosa angejua kuwa chakula hicho kilikuwa chake na nduguze. Mazoea yana taabu. Nayo siku ya kufa nyani miti huteleza. Rosa aliamini kuwa chakula kile kilikuwa cha Bi Kovu na wanawe. Kumbe ulikuwa mtego wa Bi Kovu! Rosa alijituma kwenye kazi zake kama kawaida. Mchovu na mwenye njaa maskini. Bi Kovu alijicheleweshа mtaani Kitovuni ili kuyaruhusu mambo yajiweke. Kazi ziliendelea kumzidia nguvu Rosa. Hata hivyo, kabla ya jua kukaribia magharibi alikuwa akimalizia udhia ule. Nao nduguze wakawa wametoka shuleni. Njaa ilikuwa ikiwakereketa si haba. Walikivamia chakula kile

kama mwangaza uvamiavyo giza. “Jamani tafadhali msikile kile kilicho jikoni. Ni cha mama.” Alisema Rosa kwa nduguze wakinzani. Kumbe heri asingewaambia. Ilikuwa sawa na kumwambia samaki atahadhari mto unafurika.

Dakika thelathini zilizofuata ziliipata nyumba ya Bi Kovu katika sokomoko na masikitiko yenye kina kirefu. Watoto wawili walikuwa wamelala dafrao huku mapovu yakiwatoka vinywani. Baadaye kidogo wakasimama na kuanza kusema maneno yasiyoeleweka. Akina mama wakapasua ukimya wa jioni hiyo kwa mayowe. Wachache wenye ujasiri wakasema chini kwa chini. Kunao walioona kana kwamba ni marehemu wazazi wa Rosa waliokuwa wakilipiza kisasi. Hata hivyo wachache walioujua ukweli walibaki kushangaa na kushangilia mtenda akijitenda yeye. Mama watoto aliwasili maji yakiwa yamezidi unga. Watoto wametulizwa hawatulii. Wazee wa toba na matambiko wakajaribu gangaganga zao zikagonga mwamba. Wakaingia katika chumba kimoja kilichokuwa pembeni mwa nyumba ya Bi Kovu. Baadaye walitoka na vikorokoro visivyoeleweka na vibuyu kadhaa. Aidha palikuwepo na fuvu la kichwa la mtoto mchanga hivi. Kando yake picha ya Rosa imechorwa ishara ya msalaba usoni. Wanakata wakawa vinywa wazi. Kunao walisingizia sumu kutumika kuwachachawiza watoto wale. Wengine wakadai ni miungu iliyokuwa imekasirika. Kunao waliodai kuwa kukosa elimu ndiko kulikowafanya wana wale kubadilika ghafla. Wengine wakadhani ni mababu waliokuwa wamekasirika na hivyo kuamua kuiadhibu familia ile. Almradi kila mmoja alikuwa na yake ya kuwazia. Ubongo sio maji yaliyotuama. Haukai bila mawazo. Kunao waliopiga picha na wengine kurekodi video kwa simu zao za rununu. Bila shaka habari hii ingeenea kama maradhi ya homa kali kama vile Korona. Keshoye kijiji kingefurika wanahabari wa kila aina kutafuta wa kuhoji. Nao wahojiwa wangatilia chumvi na kuongezea viungo mbalimbali ili kuikoleza habari.

“Achomwe! Achomwe! Achomwe! Mchawi achomwe! Mlaaniwa atiwe moto!” wanakijiji waliitana. Ghafla bin vu, makuti na magome makavu ya migomba yalikuwa tayari. Mafuta na kiberiti mkononi. Moto ukawa nabihi kutekeleza wajibu wake. Wakati huu wote Rosa alikuwa mkono mmoja amemshika Bi Kovu huku mwingine akiyafuta machozi yaliyokuwa yakimtoka kwa fujo. Hakujua chanzo cha matukio yaliyokuwa yakijikunjua jioni hiyo. Mama mmoja mnene utadhani

akitembea ardhi inabonyea ndiye aliyemchukua Rosa. Bi Kovu akafungwa makuti na magome yale kiunoni. Mafuta ya petroli yakamwagwa juu yake. Hapo akapiga magoti. Akaangalia angani na kusema, "Wazazi wa Rosa nisameheni. Nilitaka kuvuna nisikopanda. Nimekula nikasakamwa. Nisameheni kwa kusababisha mauti yenu kabla ya wakati wa Mungu. Naomba radhi duniani na ahera kwa kumtesa mtoto wenu na kujaribu kumtilia sihiri na sumu. Nimelipa mimi na damu yangu. Nimekataliwa naye Mungu na miungu yangu ya giza"

Mume wa nyumba alifika mke akiwa anageuka majivu. Watoto wake nao wanaota moto wa mauti wakicheka kama ni mahoka. Rosa alimkimbilia mjomba wake huyo na kumshika mkononi. Wote wakaajabia matukio yaliyokuwa yakijiweka mbele yao. Wanakijiji wakasema kwa ujasiri kwa mara ya kwanza, "Hatutakubali mambo ya uchawi na ulozi katika jamii yetu tena. Leo itakuwa mwanzo wa mwisho wa nguvu hizi za giza." Baada ya kuuota moto wa mauti, wanakitongoji walianza kuondoka mmoja mmoja. Ndipo mjombawe Rosa alipotokwa na chozi zito. Akidhani ni yeye tu na Rosa waliobaki pale, akajiuliza kwa sauti, "Jamani! Asili ya uchawi na kutakiana mabaya ni nini?" alisikia sauti ya mzee mmoja aliyebaki pale ikimjibu. "Asili ya uchawi ni visasi, tamaa, fitina na zaidi ya yote wivu." Hata wawili hao walipokuwa wakielekea kwenye karadinga la polisi ili kuandikisha matukio ya siku hiyo kituoni, Rosa alimwuuliza mjomba wake, "Mjomba, wivu ni nini? Nguvu za giza na wivu zina uhusiano upi?" mjomba aliangalia wanawe waliopagawa waliobaki wakilamba jivu la mabaki ya mama yao marehemu, kisha akamwangalia mpwawe na kumjibu, "Mwanangu, wivu ndio asili ya uchawi. Ndiposa wengine huziita nguvu za giza. Usijiulize giza lina nguvu gani. Utajisumbua bure." Tangu hapo, Rosa akawa mwoga wa giza ajabu. Asijue giza alilolizungumzia hau yake lilikuwa zaidi ya giza la usiku. Wote wawili wakaelekea kituoni kuandikisha tukio la asili ya uchawi. Pale kituoni palijaa wanahabari pakawatapika wengine nje. Bila shaka magazeti ya siku iliyofuata yengeuza kama kaimati moto gulioni. Kamera zao hazikupumua. Zilimwekamweka kwa kasi na ustadi. Nuru ya moto uliofukuza giza la wivu na hiana ikiwa maudhui makuu ya matukio ya siku hiyo. Rosa alitaka kuuliza mjomba wake tiba ya maradhi waliougua mabinamu zake maskini. Mjomba ni kama alizisoma fikra zake na kumwambia, "Mwanangu, tiba ya maradhi ya wana wangu hao ni hisani na utu. Utu ndio msingi wa mema yote mwanangu. Ndiyo nuru

ya kufukuzia giza." Mwisho wa yote ukawa mwanzo wa kila kitu. Yakini, ASILI YA UCHAWI ilikuwa wazi!

# Jinyakulie nakala hii ili kuzidi kusoma